

**KWENDA: MWENYEKITI, KAMATI YA FEDHA NA UTAWALA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI**

**KUTOKA: MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI**

TAREHE: 8 Aprili, 2022

**YAH: TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA
MWEZI MACHI, 2022.**

A: MAPATO:

**I. VYANZO VYA MAPATO YA NDANI VYA HALMASHAURI (OWN
SOURCES)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kipindi cha Julai 2021 hadi Juni 2022, Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni ilijiwekea lengo la kukusanya mapato ya **Tzs 9,106,108,000**. Kwa kipindi cha mwezi Machi, 2022 zimekusanywa **Tzs 882,333,524.21** sawa na asilimia **9.69** ya Lengo kwa Mwaka. Aidha halmashauri katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022 imeweza kukusanya Jumla ya **Tzs 6,873,196,953.86** sawa na asilimia **75.48** ya lengo la mwaka.

Taarifa mlingano ya mwezi Machi, 2022

Lengo la Halmashauri kwa mwezi Machi, 2022 ni kukusanya kiasi cha **Tzs 758,842,333.31** ambapo zimekusanywa **Tzs 882,333,524.21** sawa na asilimia **116.27** ya lengo la mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufuatao ni mchanganuo wa mlingano wa

Mapato halisi kwa mwezi Machi, 2022 kama yalivyokusanywa.

Jedwali la Mlingano: Januari 2022- Machi 2022

Na	Mwezi	Makisio	Mapato halisi	Ongezeko/Pun gufu,	(%)
1	Januari	758,842,333.51	1,061,335,474.48	302,493,141.17	139.86
2	Februari	758,842,333.51	493,240,531.42	(265,601,801.89)	65.00
3	Machi	758,842,333.51	882,333,524.21	123,491,190.90	116.27

Ongezeko la ukusanyaji kwa mwezi Machi 2022 umetokana na chanzo cha ushuru wa huduma ambacho hukusanywa kila robo mwaka (Januari – Machi) malipo haya kwa baadhi ya walipaji waliweza kulipa ndani ya robo husika. Walipaji waliosalia wa chanzo hiki matarajio ni kulipa kabla ya tarehe 10/4/2022 kama sheria inavyoelekeza.

II RUZUKU KUTOKA SERIKALI KUU:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2021/2022 Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni ilikisia kupokea Ruzuku kutoka Serikali Kuu jumla ya Tzs **32,818,771,000.00**. Kwa mwezi Machi, 2022 fedha zilizopokelewa ni Tzs **2,244,773,002.43** sawa na asilimia **6.84** ya bajeti iliyoidhinishwa.

Aidha Halmashauri ilitarajia kupokea jumla ya Tzs **2,734,897,583.33** kwa mwezi, ambapo kiasi kilichopokelewa ni Tzs **2,244,773,002.43** sawa na asilimia **82.08** ya makisio ya mwezi; Aidha halmashauri katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022 imeweza kupokea Ruzuku toka Serikali Kuu Jumla ya Tzs **20,466,787,605.34** sawa na asilimia **62.36** ya lengo la mwaka.

Ruzuku iliyopokelewa kwa mwezi Machi, 2022 ni kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapa chini.

JUMLA YA MAPATO YA RUZUKU: Januari 2022-Machi 2022

Na	Mwezi	Makisio	Mapato halisi	Ongezeko/Pungufu,	(%)
1	Januari	2,734,897,583.33	2,215,332,449.68	(519,565,183.65)	81.00
2	Februari	2,734,897,583.33	2,269,010,733.87	(465,886,849.46)	82.97
3	Machi	2,734,897,583.33	2,244,773,002.43	(490,124,580.90)	82.08

Fedha za ruzuku zilizopokelewa ni katika maeneo ya mishahara, ruzuku ya matumizi ya kawaida, elimu bila malipo kwa Shule za Msingi na Sekondari, MDH, TASAF na Basket fund

B: MATUMIZI:

Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Juni 2022 Halmashauri imekisia kutumia Tzs. **41,924,878,999.76** kati ya fedha hizo Tzs **32,818,771,000.00** ni kwenye maeneo ya Ruzuku; na Tzs. **9,106,108,000.00** ni katika maeneo yasiyo ya Ruzuku.

Matumizi halisi kwa mwezi Machi 2022, ni Tzs **2,957,173,644.43** sawa na asilimia **7.06** ya bajeti yote ya matumizi ya mwaka .Aidha matumizi ya ruzuku kwa Mwezi Machi, 2022 ni Tzs **2,213,046,174.79** sawa na asilimia **6.75** ya bajeti ya mwaka.

Matumizi ya vyanzo vya ndani kwa mwezi Machi, 2022 ni Tzs **744,127,469.64** sawa na asilimia **8.18** ya bajeti ya mwaka.

Aidha Halmashauri kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022 imeweza kutumia jumla ya Tzs **24,884,090,290.44** sawa na asilimia **59.35** ya lengo la mwaka.

Mchanganuo wa matumizi ya Fedha Mwezi Machi, 2022 ni kama ifuatavyo:

▪ Matumizi maeneo yasiyo ya ruzuku	Tzs	744,127,469.64
▪ Matumizi maeneo ya Ruzuku	Tzs	2,213,046,174.79
Jumla	Tzs	2,957,173,644.43

Matumizi yaliyofanyika ni katika maeneo ya mishahara, ruzuku ya matumizi ya kawaida, elimu bila malipo kwa elimu msingi na sekondari, MDH, TASAF, Mfuko wa pamoja wa Afya (Basket fund) na matumizi ya vyanzo vya mapato ya ndani.

Jedwali "A", "B" "C" na "D" ikionyesha muhtasari Mapato,

Matumizi, mchanganuo wa taarifa mlingano wa mapato ya ndani wa mwezi Machi, 2022 na mchanganuo wa matumizi (itemized),

Nawasilisha,

Jenoviva Meshi
**K.N.Y: MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI**